

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



• ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO •

MKUTANO WA SABA



KIKAO CHA SITINI

05 JULAI, 2017



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA SITINI – TAREHE 05 JULAI, 2017

I. DUA:

II. TAARIFA YA SPIKA:

III. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:

Maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2017 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2017*].

MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA NA SHERIA:

Maoni ya Kamati ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2017 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2017*].

MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani wa Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2017 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2017*].

IV. MASWALI:

WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:


497. MHESHIMIWA BONIPHACE MWITA GETERE (BUNDA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Miradi ya Maji ya Mgeta/ Nyang'ara na Nyamuswa/ Salama kati ambayo inadhaminiwa na Benki ya Dunia imeshindwa kumalizika tangu mwaka 2013 hadi leo:-

- (a) Je, ni lini Serikali itakamilisha miradi hiyo kwa ufanisi na kukabidhi kwa watumiaji;
- (b) Je, Serikali inatoa tamko gani juu ya ahadi ya aliyekuwa Naibu Waziri wa Maji Mheshimiwa Makala akiwa Bungeni, ya Ukaguzi wa Miradi hiyo hususan Mradi wa Mgeta ambao una bajeti mbili kwa Mradi mmoja.

498. MHESHIMIWA ESTHER NICHOLAS MATIKO (TARIME MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Wilaya ya Tarime imepakana na Ziwa Victoria na Mto Mara ambao kwa sehemu kubwa uko ndani ya Wilaya ya Tarime; licha ya kuwa karibu sana na vyanzo vya maji wananchi wa Tarime Mjini kwa muda mrefu wamekuwa wakitumia maji ya Bwawa la Nyanduruma lililoko Kata ya Kenyamanyoro lililojengwa na Mjerumani ambalo halijawahi kufanyiwa usafi tangu kuchimbwa kwake na kupelekea wananchi watumie maji yasiyo safi na salama kwa matumizi ya binadamu:-

- 
- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka maji ndani ya Mji wa Tarime kutoka Ziwa Victoria na Mto Mara kama ilivyowahi kufanya kwa kuyapeleka Shinyanga:-
 - (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuleta wataalam kukisimamia na kukiendeleza chanzo cha maji kilichopo japo hakikidhi mahitaji.

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

499. MHESHIMIWA MBARAKA KITWANA DAU (MAFIA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Ujenzi wa barabara kutoka Kilindoni – Mafia – Rasi Mkumbi kwa lami ni ahadi ya Mhe. Rais wa Awamu ya Nne, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete na Ilani ya CCM 2015 - 2020:-

Je, ni lini ujenzi huo utanza.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

500. MHESHIMIWA STELLA IKUPA ALEX (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:- Kutokana na umuhimu wa Elimu Jumuishi Tanzania (*Inclusive Education*):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa kila Mwalimu anapatiwa mafunzo maalum yatakayomuwezesha kufundisha Wanafunzi wenyewe ulemavu.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

501. MHESHIMIWA ALLY SALEH ALLY (MALINDI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:- Bunge lilipitisha Mpango wa Maendeleo na katika utekelezaji wake kasi ya Serikali kukopa imekuwa kubwa na bila shaka matokeo yake ni kuongezeka kwa Deni la Taifa:-

- (a) Je, Serikali inaweza kuliambia Bunge hili ni kiasi gani kimekopwa hadi sasa ndani na nje ya nchi;
- (b) Je, Serikali inajipangaje kulipa deni hilo pamoja na deni ambalo tayari lipo.

V. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na Kusomwa Mara ya Tatu)

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2017 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2017*].

VI. TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE:


VII. HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE:

WAZIRI MKUU.

VIII. WIMBO WA TAIFA:

DODOMA
05 JULAI, 2017

DKT. T. D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE



BUNGE LA TANZANIA